Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili 00005809 Toleo 21: Machi 2016

Huduma Bora za Afya kwa Wote

Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya ya Kondoa Mh. Omari Kariati akifungua kikao cha Baraza la Madiwani.

Madiwani: Sikika karibuni tena Kondoa!

Na Thomas Ludovick, Kondoa

Kwa kauli moja, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa limetengua uamuzi wake wa kuifungia Sikika kufanya kazi ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii katika sekta ya afya wilayani humo. Uamuzi huo ulifikiwa Februari 4 mwaka huu, baada ya Sikika kufungiwa kufanya kazi wilayani humo kwa zaidi ya mwaka mmoja (2014).

Katika kikao hicho kilichohudhuriwa na Mkuu wa Mkoa Dodoma, Chiku Gallawa, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mh. Omari Kariati aliwashukuru madiwani kwa kuridhia kuliruhusu shirika kuendelea na kazi na kusema uamuzi huo umezingatia mahitaji na maslahi ya wananchi.

Juni, 2014 Baraza la Madiwani (lililopita), lilipiga marufuku Sikika kufanya kazi katika wilaya hiyo kwa madai kwamba shirika hilo linatoa taarifa za uongo, zikiwemo tuhuma za kuwadhalilisha madiwani na kusambaza vijarida kwa wananchi vyenye taarifa zilizodaiwa kuwa si sahihi. Hata hivyo, Sikika ilikanusha madai hayo yote.

Akizungumza katika mkutano huo, RC Chiku Galawa aliwapongeza madiwani kwa kutambua umuhimu na mchango wa Sikika katika kuwezesha wananchi kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Afya wilayani humo.

“Naahidi mkoa wangu kushirikiana na Sikika na natoa wito kwa mashirika mengine kushiriki kufanya miradi mbalimbali ya maendeleo” anasema Gallawa na kuongeza kuwa “Sikika inashirikiana na Serikali kuanzia ngazi za juu hadi chini, hivyo kama mnataka maendeleo fungueni milango na wengine waje Kondoa”

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Sikika, Bw. Irenei Kiria aliwashukuru madiwani kwa uamuzi wao wa kuliruhusu shirika kuendelea kutekeleza kazi zake wilayani humo na kuahidi ushirikiano zaidi baina yao. Awali, Sikika ilifungua kesi Mahakama Kuu ili kupata kutafuta tafsiri ya kisheria iwapo Baraza la Madiwani lina mamlaka kisheria kuifukuza asasi ya kiraia katika wilaya. “…lakini kutokana na maamuzi haya mliyofanya…tunaahidi kuiondoa kesi hiyo mahakamani endapo tutapata barua rasmi inayoelezea uamuzi rasmi wa kikao hiki, hivyo kuendelea kufanya kazi rasmi kama ilivyokua hapo awali,” alisema Bw. Kiria.

Diwani wa Kata ya Saranga, Mh. Raymond Hamza alielezea kufurahishwa na uamuzi wa kurudi kwa Sikika na kusema kwamba kutasaidia kuibua matatizo na changamoto zilizopo katika huduma za afya hususan maeneo ya vijijini, ili ziweze kupatiwa ufumbuzi.

NDANI

Madiwani: Sikika karibuni tena Kondoa! 1
Wananchi Kondoa Walipongeza Baraza la Madiwani 2
Tujisahihishe, Tushirikiane Kuwatumikia Wananchi Kondoa 3
Tumejifunza nini mgogoro wa Kondoa? 4

HALIUZWI

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Lt. Chiku Gallawa akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani wilayani Kondoa.

Wananchi Kondoa Walipongeza Baraza la Madiwani

Na Nelson Lema, Kondoa

Uamuzi wa kuruhusu shirika la Sikika kuendelea kufanya kazi za ufuatiliaji na uwajibikaji kwa jamii, umepongewa na baadhi ya wananchi wa wilaya ya Kondoa kwamba umezingatia maslahi ya jamii na misingi ya utawala bora.

"Ni takribani miaka miwili sasa tangu tupokee kwa masikitiko kufungiwa kwa Sikika na Baraza la Madiwani lililopita hapa Kondoa. Baraza hili la sasa limekuwa na msimamo thabiti na kuelewa majukumu na shughuli za Sikika kupitia timu ya Ufuatiliaji Uwajibikaji Jamii/SAM. Tunaahidi tutaendelea kushirikiana vyema na madiwani, Halmashauri na wadau wengine, na pindi changamoto zinapotokea tukae kwa pamoja na kuwe na ukaribu wa sehemu zote." alisema Bw. Waziri Fataki mmoja wa wajumbe wa iliyokuwa timu ya SAM Kondoa.

Akizungumzia uamuzi huo, Bi. Shamila Ibrahimu ambaye pia ni mkazi wa Kondoa anasema, "Nimehamasika sana kusikia uamuzi wa baraza la madiwani kuirudisha Sikika. Walitusaidia sana kutetea masuala mbalimbali ya afya, mfano kusogezwa kwa huduma za kupima kinga mwilini kuja vijijini, upatikanaji wa dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI/ARV's, machine za kupima VVU, CD4, huduma hizi ziliendelea kuboreka kwa kweli."

Mwananchi mwingine, Jumanne Abdala Kiyombo alisisitiza kwamba ni wakati wa wananchi kufuatilia maendeleo yao, kutoa maoni na kusikilizwa kupitia vyombo mbalimbali. Alienda mbali na kupendekeza kuwa ikiwezekana waliosababisha Sikika kufungiwa kufanyakazi wilayani Kondoa wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kulidhalilisha shirika na kujaribu kuficha ukweli kuhusu matumizi ya rasilimali za umma.

Aziza Emmanuel Simnyamoga ni mmoja wa walionufaika na mafunzo ya SAM, yaliyokuwa yakiratibiwa na Sikika. Anasema: "Nimefurahi sana kwa kurudishwa kwa shirika kwasababu tutaendelea kujengewa uwezo kupitia zoezi la Ufuatiliaji Uwajibikaji Jamii, tutaendelea zaidi kujua haki zetu, kuzidai kwa kufuata utaratibu na mwishowe huduma za afya zitaboreshwa zaidi."

Taarifa za kuiruhusu Sikika kurejesha shughuli za kuwezesha jamii wilayani Kondoa pia zilimfikia Bw. Omari Kidima. "… zile changamoto zilizokuwa zimezorota zilizidi kurudi nyuma baada ya kufungiwa shirika, tulikata tamaa sana, tuliona watu wanapenda tukose maendeleo. Kwa sasa tunaamini changamoto hizi zitaendelea kufanyiwa kazi".

Naye mwakilishi wa kundi la watu wenye ulemavu, Acqulina Gharimo alisema "nimefurahi sana kwa maamuzi ya Baraza la sasa, lakini ni vyema madiwani na Halmashauri wawe makini na uhakika wa kina kwenye kufanya maamuzi makubwa kama haya kwa kushirikisha pande zote ili wapate ukweli ili jambo hili lisirudie kwa baadae."

Akichangia maoni yake, Bi. Salama Juma Salumu anasema "nimepokea kwa mikono miwili maamuzi mazuri ya baraza la madiwani. Matokeo ya maridhiano haya ni huduma nzuri kwa jamii kwani shirika haliwezi kufanyakazi kwa kuvutana na serikali. Mafunzo wanayotoa yanatufundisha sisi wanachi si tu kusimamia watoa huduma katika sekta ya afya bali hata kujisimamia sisi wenyewe katika maisha yetu ya kila siku. Tukumbuke kwamba lengo la SAM ni kuwawezesha wananchi kusimamia na kufuatilia rasilimali za umma kwa lengo la kuboresha huduma za jamii ikiwemo Afya.

Bi. Salama anamalizia kwa kusema, "Baada ya kujengewa uwezo katika mafunzo ya SAM 2014, tuliweza kufuatilia masuala mbalimbali ya afya ikiwemo uwepo wa dawa katika vituo vya kutolea huduma ambao ulikuwa mzuri, pia tulibaini changamoto kubwa ya upungufu wa watoa huduma katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma kwa mfano zahanati ya Kiteo na Bumbuta kulikuwa na mtoa huduma mmoja tu kwa kila zahanati."

Ni wazi kwamba mafanikio hayo na mengineyo yaliweza kufikiwa kutokana na ufuatiliaji wa karibu uliofanywa na wananchi wenyewe baada ya kupatiwa mafunzo ya SAM miaka ya 2012/14 . Wananchi wana kila haki ya kuwapongeza madiwani wao kwani wengi waliweza kunufaika kwa kujengewa ujasiri na kupanua uelewa kuhusu haki na wajibu wao katika kusimamia miradi na rasilimali za umma kupitia SAM/UUJ.

Tujisahihishe, Tushirikiane Kuwatumikia Wananchi Kondoa

Na Richard Msittu, Dodoma

Baraza jipya la Madiwani lililoanza kazi wilayani Kondoa mwaka 2016 limedhihirisha dhamira yake ya kulinda na kuheshimu uhuru, mipaka na haki za msingi za jamii. Hii imedhihirika baada ya Baraza kuiruhusu Sikika kurejesha shughuli zake katika halmashauri hiyo.

Tofauti na Baraza lililomaliza muda wake 2014, Baraza hilo limeonesha ukomavu, utashi na utayari wa kulinda maslahi ya wananchi kwa kusimamia sheria na kanuni zake, kwa kuazimia kwa sauti moja, kufuta uamuzi wa kuzuia utekelezwaji wa shughuli za Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii, zinazoratibiwa na Sikika, wilayani Kondoa.

Masuala mengine ya msingi ya kujivunia kwa Baraza jipya kama chombo cha wananchi ni jinsi walivyorejesha heshima yao na kujenga upya imani ya wananchi kwamba chombo chao ni sauti madhubuti inayoakisi uwakilishi anuwai wa jamii. Pia, kuhuishwa kwa dhana ya uwajibikaji, uwazi na ushiriki wa wananchi kunaashiria uwakala chanya wa mamlaka hiyo.

Usitishwaji wa shughuli za Sikika hususan zoezi la uwajibikaji jamii uliathiri kwa kiasi kikubwa ushiriki wa wananchi katika kufuatilia uwajibikaji kwenye upatikanaji wa huduma za afya wilayani humo.

Wananchi wa kata ya Kolo wakishiriki uchaguzi wa wajumbe wa timu ya SAM.

Kimsingi, utekelezaji wa program ya UUJ unalenga kuhimiza ushiriki wa wananchi na wawakilishi wao (madiwani) katika kusimamia uwajibikaji kwa watendaji na kukuza uwazi katika utekelezaji wa shughuli za umma.

Kauli ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, Mh. Alhaji Omari Kariati katika Baraza la madiwani la tarehe 04/02/2016, inadhihirisha jinsi wananchi walivyoathiriwa na maamuzi ya Baraza la madiwani. “Baada ya kuwaondoa Sikika kwa kweli wananchi wengi wa Kondoa walililaumu Baraza la madiwani kwa maamuzi ya kuliondoa shirika hapa wilayani”

Mh. Kariati anaeleza kwamba baada ya kuwafungia Sikika, madiwani waligawanyika kwa sababu ya mitazamo tofauti kuhusu ripoti ya UUJ. “Katika taarifa hiyo mambo mbalimbali yaliibuliwa katika sekta ya afya. Hata hivyo, Sikika ni kama kioo, hivyo Baraza hili limeona ni chombo cha muhimu sana ambacho tunakihitaji kwa kuwa wanaona mbali zaidi katika sekta ya afya kuliko sisi.”

Akiunga mkono hoja ya kurejesha ushirikiano na Sikika, Diwani wa Salanka, Mh. Rahimu Hamza alisema “kuwepo kwa Sikika kutaweza kuendelea kutuonesha mafanikio na changamoto mbalimbali katika sekta ya afya hapa wilayani. Tumeamua kwa pamoja kuwarudisha Sikika kwa kuwa uamuzi wa Baraza lililopita haukuwa sahihi na haukuitendea haki Sikika wala wananchi…baadhi ya watu waliokuwa kipindi kile walikuwa na chembe ya ufisadi, hawakupenda kumulikwa na kufikia uamuzi wa kusitisha shughuli za Sikika hapa wilayani.”
Mh. Hamza anatoa mfano wa ripoti ya SAM ya mwaka 2012, ambapo idara ya afya katika ripoti ya utekelezaji wake ilionesha shughuli ya ujenzi wa choo katika zahanati ya Khubunko kwamba ulikamilika kwa asilimia 100. “Hata hivyo, baaada ya Sikika na timu ya SAM ya wilaya kupitia hawakukuta ujenzi wowote wa choo katika zahanati ya Khubunko. Sasa hapa utasema Sikika na timu ya SAM ndio wabaya?”

Tunaamini kuwa maamuzi ya madiwani wilayani Kondoa, ni mwanzo wa ukurasa mpya wa ushirikiano kati ya halmashauri, asasi za kiraia na wananchi.

Uzoefu huu unatukumbusha maandiko ya Baba wa Taifa, Hayati Mwl. J.K Nyerere, katika moja ya nukuu zake, ndani ya kitabu cha “Tujisahihishe”: “Kosa kubwa sana ambalo pia linatokana na unafsi ni kutaja makosa ambayo sisi wenyewe hatunayo, na kuficha makosa ambayo sisi wenyewe tunayo. Hili ni kosa lile lile linalotufanya tulaumu tusiowapenda, na kutolaumu tunaowapenda, bila kujali ukweli.”

Tujisahihishe, Tushirikiane Kuwatumikia Wananchi wa Kondoa!

Mh. Khadija Kilala akichangia mada katika Baraza la Madiwani.

Tumejifunza nini Mgogoro wa Kondoa?

Na Jackson Sikahanga, Kondoa

Mvutano uliojitokeza kati ya Sikika na Halmashauri ya Kondoa umetufunza mambo kadhaa muhimu. Habari hii inaainisha kwa ufupi mafunzo ambayo Sikika, Wananchi, Madiwani na Watendaji wa halmashauri waliyapata kutokana na maamuzi ya kusitisha shughuli za shirika, ikiwemo kutoa mafunzo ya uwajibikaji jamii kwa wananchi wilayani humo:

1. Maamuzi sahihi na ya haki, yenye kuzingatia maslahi ya umma huondoa mivutano isiyokuwa na tija kwa jamii.

2. Ni muhimu kwa pande zote husika kufuata taratibu, miongozo na sheria za nchi hasa wakati wa utekelezaji wa pamoja wa majukumu yanayohusu maendeleo ya jamii.

3. Watetezi na wawakilishi wa wananchi wasimamie maslahi ya wananchi hasa pale haki yao ya kushiriki katika masuala yanayogusa maisha yao inapotishiwa ama kuporwa na baadhi ya viongozi walioko katika ngazi za maamuzi.

4. Kuwa na ujasiri wa kusimamia ukweli na haki bila kuyumbishwa na taasisi yoyote. Kitendo cha kusitisha zoezi la SAM - 2014 ambalo lilikuwa likifanywa na wananchi wa Kondoa, kilikuwa na lengo la kufinya uhuru wa wananchi wa kufuatilia mipango, matumizi, utendaji na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za afya kwa umma.

5. Wananchi wahakikishe wanashiriki katika mipango mbalimbali ya serikali kuanzia ngazi ya msingi, mfano mikutano ya jamii, ili kufahamu matumizi ya rasilimali za umma, kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

6. Madiwani, kama chombo cha usimamizi wa watendaji katika Halmashauri wasimame kidete kutetea maslahi ya wapiga kura wao na kulinda haki yao ya kupata taarifa za bajeti na mipango ya maendeleo katika maeneo yao, kushiriki katika kufuatilia na kuhoji matumizi ya rasilimali za umma.

7. Shauri lolote linalohusisha Halmashauri/Madiwani na asasi za kiraia au wadau wengine kwa manufaa ya wananchi ni vyema likatafutiwa suluhu kwa njia ya majadiliano na sio upande mmoja kufanya maamzi makubwa yasio na tija kwa jamii.

8. Muundo wa timu za wilaya za SAM kimsingi zina uwakilishi wa makundi mbalimbali ya jamii wakiwemo madiwani na watendaji wa serikali. Timu zikishaundwa, zinapaswa kufanyakazi kwa umoja katika kusimamia maslahi ya wananchi kwa ujumla na kufuata misingi ya SAM. Timu inapaswa kuwa na wajumbe waadilifu, wanaojali maslahi ya umma, ili iweze kufanya kazi bila kutumiwa kulivuruga zoezi la SAM.

9. Wananchi ndio walengwa wakuu katika matokeo ya zoezi la SAM kwani lengo ni kufikia huduma bora za jamii. Katika mvutano huo, wanajamii wa Kondoa walionesha ujasiri mkubwa kwa kutetea haki yao hususani ya kupata taarifa za utendaji, mipango na utekelezaji wa miradi ya afya pamoja na utolewaji wa huduma za afya Wilayani Kondoa.

Ni tumaini letu kwamba mafunzo hayo yatafanyiwa kazi na wahusika wote katika nafasi zao ili kuondoa tofauti zilizopo kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183 - Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57
Ujumbe Mfupi: +255 688 493 882

Nukushi: +255 22 26 680 15
Barua Pepe: info@sikika.co.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
@sikika1
Sikika Tanzania
sikikatanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Nukushi: 026 23 21316